



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI MASASI



(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Kumb. Na. MTC/B.10/I/VOL.III/ TEMP/80

Tarehe: 08/06/2023

## TANGAZO

### TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA USAFI KATIKA HALMASHAURI YA MJI MASASI.


1. Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashuri ya Mji Masasi inapenda kuwaalika kikundi au Kampuni yenye uwezo wa kufanya kazi ya Usafi katika Jengo la Utawala na Hospitali ya Mkomaindo Halmashauri ya Mji Masasi.

Koteshe kama zilivyo ainishwa kwenye jedwali,

S/N	Namba ya kotesheni	Maelezo
1	LGA/135 /2023/2024 /NC/01	kufanya kazi ya Usafi katika jengo la Utawala Halmashauri ya Mji Masasi.
2	LGA/135 /2023/2024 /NC/02	kufanya kazi ya Usafi katika Hospitali ya Mkomaindo Halmashauri ya Mji Masasi.

2. Mwombaji. Awe na sifa zifuatazo,
- Kampuni au kikundi kiwe na leseni ya Biashara husika.
  - Kampuni au kikundi kiwe na uzoefu wa muda wa miaka mitatu.
  - Kampuni au kikundi kiwe na vitendea kazi na wafanyakazi wa kutosha.
  - Kampuni au kikundi kiambatanishe Taarifa za fedha.
  - Kampuni au kikundi kiwasilishe cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi.
  - Kampuni au kikundi iwasilishe Mpango kazi.
  - Kampuni au kikundi kiwe kimesajiliwa na BRELA.

3. Wenye sifa wanatakiwa kuja kuchukua kitabu cha Zabuni katika Ofisi ya Mkuu wa kitengo cha Ugavi na Manunuzi kwa ajili ya kujaza bei kwa gharama ya Tshs 30,000 /=-.
4. Kotesheni zote zijazwe kikamilifu kwa kuanisha namba ya kotesheni na kuiwasilisha kupitia anuani tajwa hapo chini.
5. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni **15/06/2023** kabla ya saa **04.00** Asubuhi. Kotesheni zitafunguliwa Tarehe **15/06/2023** saa **04.00** Ukumbi wa Mikutano na wawakilishi wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi huo.
6. Kotesheni ambazo zitachelewa, zisizo kamilika au zilizowasilishwa katika muundo usio kubalika hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathimini bila kujali mazingira yoyote yale.



Jumanne Chaula

Kaimu Mkurugenzi wa Mji

**MASASI.**

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,  
HALMASHAURI YA MJI,  
S.L.P 447  
MASASI.**